



Mwongozo kutoka MCT: Uandishi wa Habari za Janga la Korona

Baraza la Habari Tanzania (MCT)

Utangulizi

Ni jukumu la mwanahabari kutoa taarifa sahihi na kuwa makini katika kuiarifu jamii. Wakati wa kipindi hiki kigumu mitaarafu ya afya ya binadamu ambapo tunapambana na ugonjwa wa COVID-19 (ambao pia unajulikana kama ugonjwa mpya wa homa ya mapafu—novel Coronavirus au “Korona” kwa kifupi) jukumu hili la wanahabari linapata umuhimu mkubwa zaidi. Kirusi cha COVID-19 kimeshattinga Tanzania tayari, kwa mujibu wa uthibitisho uliotangazwa na Wizara ya Afya, Mandeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Baraza la Habari Tanzania (MCT), pamoja na mambo mengine, linawajibika kuhakikisha kwamba wanahabari nchini wanazingatia viwango vya juu kabisa vya kitaaluma na kimaadili. Ili kuhakikisha vyombo vya habari nchini vinafanya kazi za kuarifu umma kwa usahihi katika kipindi cha majanga kama hiki tunachopitia sasa, MCT imetayarisha Mwongozo ufuatao kwa ajili ya wanahabari.

Mwongozo

- Pamoja na kwamba hutegemewi kupuuzia uzito wa janga lililo mbele yetu kwa sasa, unapaswa kuchangia katika kupunguza hofu na taharuki miongoni mwa jamii.
- Jitahidi kuelewa mipango na mikakati ambayo inatekelezwa katika juhudzi za kupambana na janga la Korona na athari zake kijamii na kiuchumi.
- Ongea na kuhoji watu wengi iwezekanavyo na wa tabaka mbalimbali. Jaribu kupata mitazamo anuwai ya watu wanaopitia kipindi cha tukio la janga hili ili uweze kupata mrejesho utakaowezesha uongozi wa nchi kuwa na mipango sahihi ya kupambana na janga lililopo.
- Zingatia kwa makini taratibu za kitaaluma, huku ukihakikisha unatumia vyanzo vya habari vya kuaminika kama vile Wizara ya Afya na Shirika la Afya Duniani (WHO).
- Jihadhari na taarifa potofu! Fanya juhudzi ya kuthibitisha ukweli wa taarifa ulizopata ili usiwe sehemu ya mtandao wa kuzambaza habari zizizo za kweli.
- Waheshimu waathirika wa Korona na jali haki yao ya faragha. Punguza mahojiano nao na waathirika wasipigwe picha na majina yao yasitajwe katika habari zinazowahusu, labda pale tu ambapo wangependa kutajwa ili kueleza usoefu wao ili jamii ijue bayana juu ya kadhia iliyowasibu.
- Kuripoti janga la COVID-19 kwa njia ya picha kuna umuhimu mkubwa, lakini panatakiwa umakini katika utumiaji wa njia hii ya kuripoti. Wanahabari wanapaswa kuhakikisha picha au vielelezo wanavyotumia katika taarifa zao ni sahihi na vinaakisi hali halisi iliyopo.
- Jikite katika kuripoti na si kufanya uchambuzi, labda tu pale uchambuzi wako unapokuwa umegezwa katika maoni uliyopata kwa wataalamu.
- Wahariri wawe makini katika uandishi wa vichwa vya habari. Kutohakikisha na uwepo wa utitiri mkubwa wa taarifa, ikiwa ni pamoja na ucharaka wa usambaaaji habari kuitia mitandao ya kijamii, watu wengi wanatosheka na kile wanachokiona kwenye vichwa ya habari na

kuchukulia kwamba hizo ndizo habari zenyewe.

- Tumia takwimu na vielelezo kwa umakini na usahihi kulingana na muktadha husika ili kuepusha hofu mionganoni mwa jamii.
- Epuka matumizi ya viashiria vya ubaguzi wa rangi—usihamasishe mitazamo finyu ya kibaguzi au kutoa habari kwa namna ambayo inaweza kusababisha wengine kushadidia ubaguzi.
- Chunguza kwa makini aina ya tukio ambalo umepanga kuhudhuria, ukizingatia kwamba pana amri ya Serikali inayokataza mikusanyiko ya idadi fulani ya watu.
- Kuwa mwangalifu, ukijua kwamba pana uwezekano wa wewe kukwamishwa kwenye karantini ndani ya eneo lililozuiliwa kutokana na Korona.
- Tafakari juu ya athari za kisaikolojia zitakazokutinga pale ambapo utakuwa umelazimika kuripoti ukiwa ndani ya eneo ambalo limeathiriwa na Korona, hasa pale ambapo utakuwa ukiripotia chombo chako cha habari huku ukiwa ndani na kituo cha afya, eneo lililotengwa au eneo lililo chini ya karantini.
- Hakikisha umejipanga vizuri kwa ajili ya dharura, ukizingatia kwamba kuna uwezekano wa maeneo fulani, wilaya, mikoa na hata nchi nzima kutengwa kwa njia ya karantini au kufungwa kwa mipaka baada ya kutolewa taarifa ya muda mfupi au bila kutolewa tahadhari yoyote.
- Epuka kukaa karibu na mtu ye yeyote mwenye kuonyesha dalili za kuwa na ugonjwa wa njia za hewa, kama vile kikohozi na kupiga chafya. Hakikisha unafunika mdomo na pua unapokohoa au kupiga chafya.
- Nawa mikono yako mara kwa mara kwa kutumia maji moto na sabuni. Tumia jeli au vifutio vya kuua vijidudu iwapo hakuna maji moto na sabuni, lakini hakikisha kwamba baadaye, unanawa kwa maji moto na sabuni.
- Usikaribiane sana na mtu unayemhoji iwapo anaonyesha dalili za kuumwa Korona. Umbali unaoshauriwa ni mita moja hadi mbili.
- Kuwa mwangalifu na aina ya usafiri unaotumia wakati wa kwenda kukusanya habari na kurejea ofisini. Epuka kutumia usafiri wa umma (daladala) nyakati ambazo vyombo hivi vinakuwa vimejaza abiria mpaka pomoni; na hakikisha unatumia jeli yenye viua-vijidudu wakati unashuka kwenye daladala.
- Tumia maikrofoni ya kushikilia (directional mic) ukiwa umeishika kwa mbali iwezekanavyo, badala ya kutumia maikrofoni inayoshikizwa kwenye mavazi (clip mic).
- Tumia glavu ukiwa, ama unafanya kazi, unazuru eneo lenye maambukizi ya korona kama vile kwenye kituo, au ukiwa kwenye eneo la kutolea matibabu. Yawezekana pia ukahitaji mavazi ya kujikinga kiafya kama vile suti ya kitabibu (bodysuit) na barakoa inayofunika uso gubigubi (full face mask).

- Vifaa vya kazi kama vile kamera, vinasa sauti na maikrofoni ambavyo vinatumia kwa kushirikiana, ni lazima vifutwe kwa vieuzi (sanitisers) vyenye uwezo wa kuondoa vijidudu kwa haraka kabla na baada ya kutumika, na watumiaji wa vyombo hivi wavae glavu.
- Kwa muda wote, hakikisha unanawa mikono vizuri ukitumia maji moto na sabuni kabla ya kuingia eneo lililoathirika, uwapo kwenye eneo hilo, na baada ya kuondoka.
- Iwapo utapatwa na dalili za maambukizo ya virusi vya Korona, hasa homa inayoambatana na shida wakati wa kupumua, wahi kumwona daktari. Zingatia kwamba, kama upo ndani ya eneo lililoathirika kwa kiwango kikubwa, unakuwa hatarini kukutana na wagonjwa wa COVID-19 kwenye vituo vya matibabu, na hivyo kuongeza uwezekano wa wewe kuambukizwa.
- Zingatia miongozo na maelekezo ya wataalamu wa afya wa eneo unaloishi.
- Shirila la Afya Duniani ([WHO](#)) na Wizara ya Afya Tanzania wanakubaliana kwamba si lazima kwa watu wasio na dalili za Korona kuvaa barakoa, labda tu pale utapoamriwa kufanya hivyo na mamlaka ya eneo ulipo, au kama upo katika eneo hatarishi kama vile hospitalini au pale ambapo wewe ni mwangalizi wa mtu ambaye anashukiwa ana maambukizi ya COVID-19.
- Yawezekana wanahabari ambao wamekuwa wakiripoti kutoka kwenye maeneo yenye maambukizi yaliyoshamiri kutakiwa watengwe na wenzao maofisini, au wakatazwe kuchanganyika na vyanzo vya habari, familia zao au watu wengine, kwa kipindi cha siku 14.
- Vipindi vinavyohusisha wageni studioni vyapasa kuepukwa. Kama ni lazima kuwa na washiriki ndani ya studio, basi pawe na umbali wa angalao mita moja kati ya mshiriki mmoja na mwingine. Waendesha vipindi sharti wanawe mikono kabla na baada ya kipindi na waepuke kugusa nyuso zao wakati wowote.
- Vieuzi sharti viwekwe sehemu zote za kuingilia vyumba vya habari, msisitizo ukiwekwa zaidi kwenye milango ya kuingia studio. Waendesha vipindi na wageni wa studio sharti wanawe mikono kabla ya kuingia studioni. Wasaidizi wa vipindi sharti wanawe kwa maji na sabuni kabla na baada ya shughuli nzima ya kurusha kipindi na pale itakapoonekana ni lazima, wavae barakoa na glavu, na
- Meza za kufanya uhariri, kompyuta, vichanganyio (mixers) na vifaa vingine vya kazi lazima vifutwe na vitakasa kila baada ya kipindi au shughuli ya uhariri.

Vipengele hivi vya mwongozo vimetokana na vianzo mbalimbali vya hapa nchini, vya kikanda na vya kimataifa vinavyohusu utendaji bora na salama kwa wanahabari ndani ya mazingira hatarishi.

Dar es Salaam, Machi 20, 2020